REPUBLIC OF KENYA

COUNTY ASSEMBLY OF LAIKIPIA

THE HANSARD

Tuesday, 17th December, 2024

The House met at the Assembly Chambers at 3.10 p.m.

[Temporary Speaker (Hon. Mary Gathoni) in the Chair]

PRAYERS

PROCEDURAL MOTION

ADJOURNMENT OF THE COUNTY ASSEMBLY

Hon. Stephen Ndiritu: Madam Speaker, I beg to move the following motion on behalf of Hon. Gichuki;

THAT pursuant to Standing Order No. 28(1), the County Assembly do adjourn until Tuesday 11th February, 2025.

Madam Speaker, this is a motion on Adjournment until February because we have to go for a long recess in accordance with our calendar. In that time, we will have Christmas and New Year and we are supposed to join other faithful to participate. I therefore urge Members to support and call Hon. Kamara to second. Thank you.

Hon. Benson Kuria: Asante, Bi. Spika kwa sababu nimeona ukweli huu ni mwaka wa baraka ikiwa tutaweza kufunga Bunge tukiwa pamoja na wewe na ukiwa Spika wetu. Ninaunga mkono mswada wa Mheshimiwa wa kutoka Thingithu Mheshimiwa Ndiritu. Ninajua ya kwamba waheshimiwa walio mahali hapa hawakuweza kusherehekea Jamhuri na wananchi ambao waliweza kuwachagua katika wodi zao.

Mheshimiwa Spika, ninafahamu vizuri ya kwamba tunaelekea kwenye msimu wa Krisimasi ambao ni msimu ambao kila mtu anasherehekea pamoja na familia yake na marafiki. Ningependa kusema ya kwamba hii ni nafasi nzuri kuunga huu mswada kwa sababu ninajua ya kwamba fikira na mawazo mengi ziko na Waheshimiwa hapa kama kupanga maneno ya Krisimasi na mwaka mpya.

Nikiunga mkono ninajua ya kwamba sote tuko hapa kwa sababu ya kujiandaa kwa sababu kutoka Januari mpaka sasa hivi, tumefika kwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu. Tukienda kuzaliwa pamoja na Yesu, tukijua ya kwamba tumefunga Bunge mpaka tarehe kumi na moja, ninaunga mkono. Waheshimiwa hapa wataweza kwenda kunena na wananchi ambao waliweza kuwafikisha mahali hapa.

Nami nikinena na wale walikuja kwa chama katika Jimbo la Laikipia, niko na furaha nikijua ya kwamba huu ni mwaka wa pili ama wa tatu ambao ninaingia. Ninaunga mkono nikijua ya kwamba sisi sote tukikuja hapa tarehe 11 Februari, tutakuwa Wangwana na hatutakuwa na mkazo ili tuweze kuingia kwenye mwaka wa 2025 tukiwa na mambo mazuri. Ninawatakia Krisimasi njema na mwaka mpya wenye baraka na manufaa mema katika familia zenu. Asante sana, Mheshimiwa Spika.

(Question proposed)

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

Temporary Speaker (Hon. Mary Gathoni): You may now debate. Hon. Kanyutu.

Hon. Simon Kanyutu: Bi. Spika, ninasimama kuunga mkono na ninashukuru kwa vile ninajua tunaelekea msimu wa Krisimasi na mwaka mpya. Ninajua tutakuwa na sherehe na mwaka ujao tutakuwa na maendeleo ya manufaa. Ninaunga mkono.

Hon. Salim Edung: Ninashukuru Bi. Spika kwa kunipatia nafasi kwa sababu katika mjadala ambao uko katika Bunge hili, ni wa kuvunja Bunge kwa muda mfupi. Tuko na wakati wa kwenda mashinani kukutana na wapiga kura ambao walitupatia kura na kuangalia maendeleo ambayo tumefanya huu mwaka na tuangalie kama maendeleo ambayo tulifanya iko katika njia ambao inastahili.

Pia ni njia moja ya kujumuisha wananchi pamoja na Wabunge katika Kaunti ya Laikipia kujua vile maendeleo inaendelea katika wadi zao. Pia tutajumuika na marafiki kwa sababu ya Siku kuu ya Krisimasi na mwaka mpya. Ninatakia Wabunge wenzangu siku kuu njema na mwaka mpya.

Hon. Salim Edung: Jambo lingine ni kwamba tunapoenda Krisimasi, kuna mambo mengi katika Krisimasi, na ni vizuri tuwe kielelezo chema. Kuwa wanaoenda mbali. Wengine wamekaa katika mtaa huu kwa muda mrefu bila kuona familia zao kwa mfano, Mheshimiwa Kamara na Mheshimiwa Lekopien. Watapata nafasi nzuri sana ya kukutana na wapiga kura katika wadi ya Sosian na sehemu nyingine, kwa sababu wako mbali sana.

Vilevile, nawatakia wafanyikazi wote katika Bunge hili na Laikipia nzima Krisimasi njema na mwaka mpya wenye ufanisi, na Mungu awabariki. Mtakapoenda nyumbani, pelekeni salamu, na Mungu awabariki wote. Asanteni.

Temporary Speaker (Hon. Mary Gathoni): I call upon the mover to reply.

Hon. Stephen Ndiritu: Asante, Bi. Spika. Nataka kuwashukuru wote ambao wamechangia katika huu mswada. Ni mswada mzuri unaoeleza vizuri hali tunayoendelea nayo. Naomba Wabunge wote walio hapa wawe na Krisimasi njema, Yesu azaliwe katika mioyo yao. Tukutane katika mwaka mpya wa 2025 ambao tunaomba uwe wa mafanikio kwa wote wanaofanya kazi katika Bunge hili, Kaunti ya Laikipia na Kenya nzima kwa jumla. Nawatakia Krisimasi njema na mwaka mpya wenye mafanikio. Tutaonana tarehe 11 mwezi wa Februari, Mwaka wa 2025. Ahsante, Bi. Spika.

Temporary Speaker (Hon. Mary Gathoni): For clarity purposes, pursuant to Standing Order No. 28(1), the County Assembly adjourns until Tuesday, 11th February 2025. Standing Order No. 29(3) states;

> *"On a day when the Assembly is scheduled to a day other than the next normal sitting day in accordance with the Assembly calendar, the Leader of the Majority Party or the Leader of the Minority Party or another member of the House Business Committee shall move a Motion of adjournment which shall be debated for not more than three hours after which the Assembly shall adjourn without question put."*

ADJOURNMENT

Temporary Speaker (Hon. Mary Gathoni): The sittings of this House now stand adjourned until Tuesday, 11th February 2025 at 10.00 a.m.

The House rose at 3.19 p.m.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*